WATENDAKAZI WAZAWA TANZANIA

*Re-aranged and translated by Pastor Stephen Letta*

**Damari Namdori Kangalu Sefue, (1913-1976)**

Damari Namdori Kangalu Sefue alikuwa mwanamke wa kwanza wa Tanzania kupata cheti cha ualimu. Damari aliwahimiza wanawake vijana kwenda shule, akionyesha kuwa wanawake wanaweza kufaulu wakipewa fursa.

Sefue alilelewa katika familia ya wake wengi yenye wake wanne. Alikuwa binti wa pekee wa mke wa nne, Nacharo. Wazazi wake walifuata dini ya kitamaduni ya Kiafrika, wakiabudu mababu. Mwanzoni mwa miaka ya 1920, yeye na kaka zake Samiji, Mtango, na Seware walikwenda Shule ya Misheni ya Suji, ambapo waliongokea Uadventista.

Shule ilimpangia Sefue kuishi na familia ya Yosefu Mhero na Kajiru kama walezi wake. Kwa kuwa Suji ilikuwa katika nyanda za juu, ni dhahiri hali ya hewa ya huko ilikuwa ya ya baridi kali. Ingawa alilazimika kuvaa sare nyepesi na miguu isiyo na kiatu, hakuona shida, kwani alijiona kuwa amebarikiwa kwa sababu alilazimika kutembea nusu kilomita hadi shuleni, ikilinganishwa na wanafunzi wenzake ambao walilazimika kutembea hadi kilomita tatu ili kufika shuleni. Alilazimika kujitafutia kuni kwa ajili ya kupikia chakula, na usiku hapakuwa na taa za kusomea. Licha ya changamoto hizo, alitamani sana kusoma. Uchapakazi wake ulimfanya afanikiwe katika utendaji wake wa kitaaluma.

Ingawa wanawake wengi walikuwa wamesoma Suji tangu ilipofunguliwa mwaka wa 1906, mwaka wa 1924 Spencer George Maxwell alianza msisitizo maalum wa kutokomeza kutojua kusoma na kuandika. Mnamo 1927, ilikuwa lazima kwamba wanafunzi wa kike wachukue masomo ya uchumi wa nyumbani, na shule ya bweni ya wasichana ilianzishwa kwa msukumo wa Winnifrida Clifford, mwalimu mkuu kutoka Uingereza. Sefue alijiunga na Chuo cha Mafunzo ya Ualimu cha Suji, na mwaka 1931 akawa Mtanzania wa kwanza asilia kupokea cheti cha ualimu. AAM Isherwood, aliyekuwa Mkurugenzi wa Elimu wa kikoloni wa wakati huo, aliandika barua iliyosema, "Damari Kangalu hakika ni msichana wa kwanza kupata Cheti cha Ualimu cha Daraja la II, na sina budi kukupongeza kwa niaba ya Idara. Misheni yako inaweza kujivunia kuwa imeweka alama muhimu kama hii katika maendeleo ya elimu ya wanawake."

Kiu ya Sefue ya kusoma ilimfanya kuwa alama ambayo elimu ya Waadventista imechangia Tanzania. Alipata umaarufu nchi nzima, kiasi kwamba shule ya wasichana ya Tabora ilitaka kumwajiri kwa vile alikuwa mwalimu pekee wa kike wa Kiafrika katika nchi nzima. Hakuweza kwenda Shule ya wasichana Tabora, kwa sababu, kama msichana, hangeweza kusafiri mbali sana kwa kuhofia usalama wake, na badala yake alifundisha katika Misheni ya Suji kwa miaka minne.

**Maisha ya Baadaye**

Mwaka 1936 Damari aliolewa na Yohana Mpeho Sefue, mgane ambaye alikuwa chifu. Ingawa alikuwa mdogo kwa umri ikilinganishwa na mume wake, walibarikiwa kupata

watoto saba. Watoto wao walibarikiwa ambapo mmoja alikuwa mchungaji, mwingine katibu mkuu wa serikali, walimu watatu, muuguzi mmoja na mjasiriamali mmoja.

Kwa sababu ya mahitaji ya kulea familia ya chifu, Sefue aliacha huduma ya ualimu na kujikita katika majukumu yake ya nyumbani. Alielimisha watoto wake sio tu katika masomo ya shule, lakini pia masomo ya kidini ambayo yalikuwa muhimu kwa maendeleo yao. Alimsaidia mumewe katika kuweka kumbukumbu, kuhifadhi na kutunza kumbukumbu rasmi, na kuwahudumia wageni rasmi waliomtembelea mumewe.

Ingawa aliacha ualimu, Sefue aliendelea kwa bidii kuifundisha jamii jinsi wanavyoweza kuboresha kiwango chao cha maisha na malezi bora kwa watoto wao. Damari alikuwa na bidii zaidi katika kanisa lake, akihudumu kama kiongozi wa chama cha Dorkasi, akiwaongoza wanawake wengine katika kuwasaidia wenye uhitaji katika kijiji chao. Alikufa mnamo Julai 1976, akiwa na umri wa miaka 63.

**Mchango wake**

Damari Namdori Kangalu Sefue, anakumbukwa kwa juhudi yake ya kusaka elimu katika mazingira ya kikoloni ambapo wanawake walionekana kama wasiohitaji na wasioimudu elimu. Damari alikuwa chachu ya wanawake wengi kutambua umuhimu wa elimu kutokana na mafanikio ya Damari ambaye ameingia kwenye kumbukumbu kama mwanamke wa kwanza Mtazania kupata daraja la ualimu.